

Utendaji wa Wahusika wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya *Safari ya Prospa*

Saumu Mkomwa
Mhadhiri Msaidizi, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini

saumumkomwa77@gmail.com

Ikisiri

Suala la utendaji wa wahusika ni muhimu sana, na kutokana na umuhimu wake limewashughulisha watafiti mbalimbali, hususani katika fasihi simulizi na tamthiliya. Kwa kuwa wahusika husema, hutenda na hufikiri au kushindwa kufanya jambo, ni wazi kuwa utendaji sio lazima uwe katika fasihi simulizi au tamthiliya kwani hata wahusika wa riwaya hufanya mambo yote hayo. Kwa mantiki hiyo, makala hii imelenga kufafanua utendaji wa wahusika wakuu wa fasihi ya watoto ya Kiswahili kwa kurejelea riwaya ya *Safari ya Prospa* (Lema, 2004). Utendaji unafafanuliwa kwa kuzingatia mazungumzo baina ya wahusika na masimulizi ya mwandishi yanayoendana na mazungumzo hayo. Makala hii ni sehemu ya utafiti uliofanyika kwa lengo la kutunukiwa Shahada ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Data za utafiti huu zilipatikana maktabani na uwandani. Sampuli ya watafitiwa ilipatikana kwa kutumia usampulishaji lengwa kwa sababu watafitiwa walikuwa na sifa za kipekee. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa mwegamo wa kimaudhui kwa kuwa utafiti uliofanyika ni wa kitaamuli. Nadharia ya Saikochanganuzi ilitumika katika mchakato mzima wa utafiti. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa utendaji wa wahusika katika riwaya hii umetumika kwa mtindo wa kuhoji, kushawishi, kujifunza, kujenga maelewano na kuamuru. Hivyo basi, watafiti wengine wanaweza kufanya utafiti kama huu kwa kutumia riwaya nyingine za watoto.

Dhana za Msingi: fasihi ya watoto, utendaji, wahusika, riwaya

Utangulizi

Utendaji ni ufanyaji shughuli fulani; utekelezaji (Bakhressa, 1992). Maana hii hurejelea mazingira ya kawaida ambapo watu hufanya shughuli mbalimbali kama vile kilimo, michezo, na ufugaji. Shughuli hizi wakati mwingine hutumika kama sehemu ya kipato cha kujikimu. Hata hivyo, kuna mielekeo tofauti ya utendaji katika maisha yetu ya kila siku na jinsi unavyojitokeza katika kazi za kisanaa, ikiwemo fasihi. Mathalani, Mlaga (2017) anataja sanaa tendaji kuwa ni ufundi na uzuri unaotokana na utendekaji wa vitendo tu peke yake, au utendekaji wa vitendo pamoja na maneno. Anazigawa sanaa hizi katika makundi mawili, sanaa tendaji za jadi na sanaa tendaji za Kimagharibi. Sanaa tendaji za kijadi ni zile ambazo ziliibuka katika jamii za Kiafrika kama vile; utambaji hadithi, majigambo, ngoma, matambiko na miviga. Anasisitiza kuwa katika shughuli hizi watu hufanya vitendo vya kisanaa kama vile upigaji muziki, uimbaji, uchezaji ngoma na utongoaji mashairi, vikiambatana na matendo ya mwili na matumizi ya lugha. Kwa upande mwingine, sanaa za Kimagharibi hurejelea sanaa zilizojitenga na maisha ya kila siku ya watu (Waafrika) na huwa na sehemu mahususi ya iliyoandaliwa kwa ajili ya sanaa hiyo. Naye Munyioki (2018) anafafanua utendaji katika fasihi kuwa ni mchakato wa uwasilishaji wa tukio linalohusu maisha ya binadamu mahali popote pa kuigizia mbele ya hadhira. Unajumuisha kile ambacho wahusika wanasema, wanatenda, wanafikiri, na, wakati mwingine, hata kile wanachoshindwa kukifanya. Maelezo ya Munyioki yanaonesha kuwa wahusika ni nguzo muhimu katika kufanikisha utendaji kwenye kazi za kifasihi. Aidha, Njogu & Chimera (1998), na Wamitila (2002) wanafafanua kwamba wahusika katika kazi ya fasihi ni viumbe wanaoweza kuwa binadamu au wanyama wenye kuteuliwa au kusukwa kwa namna fulani kwa lengo la kuwasilisha baadhi ya sifa za

binadamu. Kwa vile wahusika ndio watendaji wakuu katika kazi za kifasihi, tunatarajia kuwa watakuwa wanatenda kutokana na kile ambacho mwandishi amedhamiria kuiambia jamii yake. Hivyo, uingizwaji wa vipengele vya kiutendaji katika fasihi ni mojawapo ya mikakati anayoitumia mwandishi kuwaumba wahusika wake ili kutimiza lengo lake kwa hadhira lengwa.

Katika makala hii, utendaji unafafanuliwa kwa kutumia lugha ya mazungumzo (dayalojia) baina ya wahusika wakuu wenyewe kwa wenyewe au wahusika wakuu na wahusika wengine, na kwa kutumia masimulizi ya mwandishi yanayokwenda sambamba na mazungumzo hayo. Kwa mujibu wa Nkwera (1989), mazungumzo baina ya wahusika yakiandikwa, hupambanuliwa kwa alama za usemi, “...” (kufungua na kufunga usemi). Mratibu wa mazungumzo hayo ni mwandishi au mtunzi. Waandishi wengi hutumia lugha ya mazungumzo ili wasimchoshe msomaji ambaye, kwa muktadha wa makala hii, ni mtoto wa miaka kumi na mitano hadi kumi na minane. Lugha ya mjazo, mara nyingi, huchosha, lakini inapowekwa lugha ya mazungumzo, mtoto anakuwa miongoni mwa wahusika wa hadithi inayosimuliwa. Mazungumzo huibua mitindo mbalimbali ya utendaji kutokana na mahitaji ya wahusika. Kwa jumla, wahusika hutenda kulingana na tukio linalowasilishwa, linaweza kuwa la furaha au kusikitisha. Utendaji huakisi lile aliwazalo mwandishi katika kazi ya fasihi.

Hata hivyo, wataalamu mbalimbali wametafiti au kuandika kuhusu utendaji. Mathalani, Wa Thiong’o (1986) anabainisha kuwa utendaji sio lazima uwe na mahali fulani pa kuigizia kwani hata katika maisha ya kawaida watu hutenda mambo mbalimbali kwa kujua au kutokujua. Mlama (1981) amedhihirisha utendaji katika tukio la Digubi ambalo huhusisha watazamaji,

watendaji na tukio linalotendwa. Naye Mbunda (1996) ameonsha uhusiano baina ya riwaya na tamthiliya kwa kusema kuwa zote zinaingiliana katika vipengele vingi. Amevitaja vipengele hivyo kuwa riwaya na tamthiliya zote zinaelezea kisa fulani. Pia, tanzu zote mbili zina matukio ambayo huzua mtiririko wa aina yake: zina wahusika ambao ndio wajenzi wa hayo matukio, zina mandhari ambayo hutoa mazingira yenye kukidhi makusudi yake na zote mbili zina lugha ambamo ndani yake dhamira ya mwandishi hujitokeza.

Finnegan (1970) anabainisha kuwa utendaji ni uti wa mgongo wa fasihi simulizi, na, hivyo, ni kijenzi muhimu katika kuzielewa kazi hizo. Hapa, anamaanisha kuwa fasihi simulizi imefungamanishwa na utendekaji kama ilivyo kwa kazi yoyote ya drama. Nyambura (2014) amevijadili vipengele vya utendaji katika tamthiliya za *Kimya Kimya Kimya* na *Sudana* kuwa vinajumuisha mandhari, maleba, uangazaji, maelekezo ya jukwaa, sauti, miondoko, mihimili, na kimya. Baadhi ya vipengele walivyovibainisha vinadhihirika pia katika riwaya, hususani riwaya ya *Safari ya Prospa*, ambavyo ni msingi wa utendaji katika riwaya.

Maandiko haya yanaonesha dhahiri kuwa suala la utendaji ni mahususi katika sanaa za maonesho kama vile tamthiliya (drama) na nyimbo. Suala la utendaji katika riwaya, hususani riwaya za watoto halijapewa upekee wake. Kwa hiyo, makala hii inatarajiwa kuziba pengo hili kwa kufafanua mitindo mbalimbali ya utendaji wa wahusika wakuu wa fasihi ya watoto ya Kiswahili, kwa kurejelea riwaya ya *Safari ya Prospa*. Kwa jinsi riwaya hii ilivyosukwa, inafaa kwa fasihi ya watoto kwa sababu imekidhi vigezo vya kuitwa fasihi ya watoto. Kwa mujibu wa Bakize (2013), fasihi ya watoto ni kazi ya sanaa inayosawiri tajiriba na maisha ya mtoto. Anaongeza kuwa

wahusika wakuu wa kazi hizo lazima wawe watoto, na lugha ilingane na kiwango cha mtoto. Vigezo anavyovitaja Bakize vinapatikana katika riwaya inayoshughulikiwa katika makala hii. Kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mtoto anatambulika kama mtu yeyote mwenye umri wa miaka sifuri hadi kumi na minane. Piaget amegawa makuzi ya mtoto kiakili katika makundi manne; kundi la kwanza linaanzia pale mtoto anapozaliwa hadi miaka miwili, kundi la pili linaanzia miaka miwili hadi saba, kundi la tatu linaanzia miaka saba hadi kumi na moja, na kundi la nne linaanzia miaka kumi na moja na zaidi (Huitt & Hummel, 2003). Hata hivyo, utafiti uliofanyika umezingatia umri wa mwisho wa utoto, yaani miaka kumi na mitano hadi kumi na minane, ambao kwa Tanzania, mara nyingi, mtoto wa umri huu anakuwa katika elimu ya sekondari. Lengo la kutumia umri huo ni uwezo wao kiakili katika kuchambua mambo ukilinganisha na umri mwingine wa utoto.

Muhtasari wa riwaya ya *Safari ya Prospa*

Makala hii imechambua riwaya ya *Safari ya Prospa* ambayo imeandikwa na Bi. Elieshi Lema na kuchapishwa na *E&D Limited* mwaka 2004. *Safari ya Prospa* inahusu kutoweka kwa Merisho, mtoto mwenye umri wa miaka minne. Merisho alikuwa mtoto wa pekee wa mwalimu Josefina na mpwa wa Prospa. Mazingira anayopotelea Merisho ni ya kutatanisha sana. Hivyo, Prospa na Josefina wakishirikiana na askari walifanya juhudi za kumtafuta bila mafanikio. Kwa hiyo, Prospa anaamua kujitosa kwenye ulimwengu wa upelelezi na kwenda Dar es Salaam kumtafuta ndugu yake. Katika safari yake, anaongozana na Sara ambaye alijitolea kumsaidia. Safari yao inakumbwa na vikwazo vingi, lakini hawakati tamaa. Wanapoingia katika jiji la Dar es Salaam, wanakutana na watoto wa mitaani maarufu kama

changudoo na kushawishika kuungana nao. Kundi hili kwa pamoja wanaungana kumtafuta Merisho. Jambo la kwanza, wanamtafuta mjomba wake Prospa aliyetitwa Feliksi, ambaye anawapeleka nyumbani kwake. Nyumbani kwa Feliksi wanamkuta Uzuri anayefanya kazi za ndani. Wanamshauri Sara ajenge urafiki naye ili kupata taarifa zitakazowasaidia kumpata Merisho. Lengo lao linatimia baada ya Uzuri kueleza kila kitu kuhusu jirani yao aliyeiba mtoto wa kiume kwa kuwa alikuwa na watoto wa kike tu. Hivyo, Merisho anapatikana kupitia vijana hao ambao walienda nyumbani kwa Mzee Mchau wakati wa usiku. Hii ni riwaya ya watoto kwa kuwa imesheheni sifa mbalimbali za fasihi ya watoto, hasa matumizi ya wahusika wakuu ambao ni watoto. Pia, riwaya hii inafaa kutumika kwenye makala hii kwa kuwa ndani yake mna vipengele mbalimbali vya kiutendaji vinavyodhihirishwa na wahusika wakuu.

Safari ya Prospa ina wahusika wakuu wawili (mmoja wa kike na mwingine wa kiume). Mhusika wa kwanza ni Prospa, kijana mwenye umri wa miaka kumi na miwili. Prospa ni mdogo wake Josefina ambaye alikuwa anaishi naye katika kota za wakata miwa wa TPC. Prospa alizoea kucheza mpira na watoto wenzake katika uwanja wa TPC kila alipotoka shuleni. Mwandishi amemchora Prospa kama mhusika aliyesababisha Merisho kupotea baada ya kumuacha alipokwenda kucheza mpira. Pia, mwandishi anampa Prospa jukumu la kumtafuta Merisho pale TPC na baadaye katika jiji la Dar es Salaam. Prospa anapanga safari ya kumtafuta mpwa wake yeye mwenyewe bila kumshirikisha dada yake. Anasafiri bila kujua atafikaje Dar es Salaam, lakini anapokutana na Sara, anapata mwanga zaidi katika safari yake, hatimaye, yeye, Sara na watoto wengine wa mtaani, wanafanikiwa kumpata Merisho.

Mhusika wa pili ni Sara ambaye ni binti mwenye umri sawa na Prospa aliyekuwa anaishi Same na bibi yake baada ya wazazi wake kufariki. Sara anakutana na Prospa katika mazingira ambayo hayatabiriki na kumwomba aongozane naye katika safari yake. Lengo la kuibuliwa mhusika huyu ni kumpa Prospa msaidizi ambaye atakwenda naye Dar es Salaam. Sara anasaidia kupatikana kwa Merisho baada ya kuwa mshauri mkubwa kwa Prospa. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa ujasiri na wepesi wa akili uliodhihirishwa na wahusika hawa ni ujumbe mahususi kwa jamii yetu kuwa, mara nyingi, watoto wadogo huwa pia wanayo hekima inayosaidia kusuluhisha matatizo mbalimbali katika jamii.

Nadharia ya Utafiti

Utafiti uliozaa makala hii ulitumia Nadharia ya Saikochanganuzi iliyoasisiwa na Sigmund Freud (1856 - 1939). Freud aliamini kuwa kila binadamu ana sehemu inayojulikana kama ung'amuzibwete wa kibinafsi. Sehemu hii huhifadhi fikra na mawazo hasi ambayo hayahitajiki katika jamii. Mawazo hayo hujitokeza kiishara katika ndoto, sanaa na utani. Nadharia hii imejikita katika nafsi tatu zinazopatikana katika akili ya mwanadamu. Nafsi hizo ni: nafsi ya kiwango cha msingi (*Id*), nafsi ya kiwango cha kati (*Ego*) na nafsi ya kiwango cha ukomavu (*Superego*). Nafsi ya kiwango cha msingi hurejelea matamano na misukumo ya mwanadamu bila urazini kama shari, hali ya unyama, na ashiki dhidi ya dhamiri. Nafsi hii ndiyo inayobeba mawazo hasi ambayo baadaye hutolewa kwa njia ya ndoto au sanaa. Matahalani, katika fasihi, kama kazi ya sanaa, inaaminika kuwa mwandishi huandika yale ambayo yalihifadhiwa katika sehemu hii kutokana na kufungwa na mila na desturi za jamii husika. Nafsi ya kiwango cha kati hurejelea matendo yenye utashi, urazini, tafakuri, na huongoza maamuzi ya busara. Katika nafsi hii ujumbe uliohifadhiwa katika

ung'amuzibwete hufupishwa kwa namna inayokubalika katika ung'amuzi wa akili ya binadamu. Kwa upande mwingine, nafsi ya kiwango cha ukomavu ni nafsi ya kidhamira na kimaadili inayochunguza uadilifu wa tendo, wema na ubaya wake, kabla ya kulitenda. Sehemu hii, yale mawazo yaliyofupishwa, hubadilishwa na kuwasilishwa kwa namna nyingine. (Vice, 1990; Wamitila, 2002; na Mbarouk, 2009). Kwa mujibu wa nadharia hii, michakato ya akilini ndiyo inayomfanya mtu atende vile atendavyo. Michakato hiyo hutokana na nafsi hizi tatu ambazo huwasukuma wahusika kutenda.

Nadharia hii ina mihimili mitatu; wasiwasi, matamano na mahitaji. Wasiwasi ni dukuduku na mashaka kuhusu maisha kwamba mtu atafanikiwa au la. Matamano hurejelea starehe hasa za kingono, na mahitaji ni yale mambo ya msingi kama chakula, mavazi na malazi, ambayo kama yakikamilishwa humfanya mtu aishi vizuri. Katika mambo haya matatu nafasi kubwa hutawaliwa na matamano (Wamitila, 2008) Kwa hiyo, kila binadamu hufanya jitihada kuhakikisha anakamilisha matamano yake. Kwa kuwa wahusika ni wawakilishi wa binadamu, basi nao hufanya jitihada ya kukamilisha matamano yao kwa upande mmoja, na matamano ya mwandishi kwa upande mwingine (Wafula na Njogu, 2007). Mambo haya matatu hupatikana katika nafsi ya binadamu, na hudhihirika kupitia matendo yao. Pamoja na mihimili hii mitatu, makala hii imetumia mhimili wa matamano, ambao kwa kiasi kukubwa huwasukuma wahusika kutenda vile atendavyo ili kukidhi matamano yao. Hivyo basi, Nadharia ya Saikochanganuzi imesaidia katika kuonesha utendaji wa wahusika, kwani wahusika hufanya maamuzi ya busara, na hutenda kwa kuangalia wema na ubaya wa tendo kabla ya kulitenda kutokana na matamano yao.

Methodolojia

Makala hii ni zao la utafiti wa uwandani na maktabani Mtafiti alikusanya data za maktabani kwa kusoma riwaya ya *Safari ya Prospa* na kumakinikia zaidi wahusika na utendaji wao. Data nyingine zilikusanywa uwandani kwa kufanya mahojiano na mwandishi wa riwaya teule na wataalamu wawili wa fasihi ya watoto. Sampuli hii ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji usio nasibu wa kipekee, kwa sababu sampuli iliyotafitiwa ilikuwa na sifa za kipekee za kuchaguliwa na kutoa data zilizokusudiwa. Sampuli hii ilitupa data zinazohusiana na wahusika na utendaji, hivyo kuwa ithibati ya data zilizopatikana maktabani. Katika zoezi la kukusanya data mtafiti alitumia mbinu ya usaili kwa mwandishi wa riwaya teule na wataalamu wa fasihi ya watoto. Pia, mbinu ya usomaji matini ilitumika kusoma riwaya hiyo. Zoezi la mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti lilifanyika kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Kothari (2004) anasema kuwa uchambuzi wa kitaamuli huwasilisha data kwa njia ya maelezo pasi na kutumia takwimu.

Matokeo ya Utafiti

Data za utafiti zimedhihirisha kuwa, kwa kiwango kikubwa, utendaji wa wahusika unajitokeza kwa njia ya mazungumzo au majibizano. Kwa mujibu wa Munyioki (2018), lugha ya majibizano hutumika kutekeleza majukumu ya kuliwaza, kupasha habari, kuhoji, kuendesha mashitaka, kuhamasisha hata kushawishi. Makala hii inajadili utendaji katika mtindo wa kuhoji, kushawishi, kujifunza, kujenga maelewano na kuamuru.

Utendaji kwa mtindo wa kuhoji

Kupitia mazungumzo, wahusika huweza kuuliza maswali mbalimbali ili kupata taarifa ambazo zinaweza kuwasaidia katika maisha yao. Maswali

hayo huulizwa na wahusika wenyewe au watu wanaowazunguka. Mathalani, baada ya Prospa kuhisi kuwa Merisho anamwita, alicheza mpira kidogo, lakini baadaye aliacha na kwenda kumwangukia. Alipofika nyumbani, aliangukia kila mahali bila mafanikio. Jambo hili lilimpa wasiwasi, akakata shauri kuwafuata watoto waliokuwa nje ya uwanja wakicheza ili ajaribu kuwahoji kama walimwona Merisho. Mahojiano yao yalikuwa kama ifuatavyo:

“Merisho yuko wapi? Mmeshamuona Merisho?” Moyo ulikuwa ukimpiga kwa nguvu kifuani. Mtoto mmoja alimjibu, “Merisho alikuafuata uwanjani.” “Lini? Alifuata wapi?” Prospa aliuliza. “Uwanjani ulipokuwa unacheza mpira,” Mtoto mwingine alisema bila kumtazama Prospa. “Mbona sikumwona?” Prospa alijiuliza. Alimwendea yule mtoto aliyemjibu bila kumtazama, akamshika shati na kumtikisa ili amsikilize vizuri. “Hebu niambie vizuri bwana,” Prospa alimkazania. Mtoto huyo jina lake Mustafa alisimama, akamtazama Prospa, akasema, “Usinirarurie shati yangu.” Alikaa tena akaendelea na shughuli yake ya kuunda gari ya bati na matairi yake ambayo alikata kutoka soli ya ndala iliyochakaa. “Mustafa niambie. Niambie basi,” Prospa alimbembeleza. “Kamtafute uwanjani huko,” Mustafa alisema ... (uk. 3 - 4).

Katika mahojiano hayo, Prospa alikuwa na shauku kubwa ya kujua mahali alipokwenda Merisho, ndiyo maana alikuwa akiuliza maswali mfululizo. Aliamini watoto waliokuwa wanacheza wanaweza kufahamu mahali alipo. Bakize (2020)¹ anasema kuwa, ukimsoma vizuri Prospa, utagundua alikuwa amepanick alipogundua kuwa Merisho ametoweka. Mwandishi wa makala hii anakubaliana na maelezo ya Bakize kwani Prospa alikabidhiwa jukumu

¹ Mahojiano kati ya mtafiti na Leonard Bakize yalifanyika katika ofisi ya mtaalamu huyu iliyopo katika jengo la TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mnamo tarehe 12/02/2020. Bakize ni Mhadhiri Msaidizi na mwandishi wa kazi mbalimbali za fasihi. Pia, ni mtafiti aliyebobea katika fasihi ya watoto.

la kuwa pamoja na Merisho wakati dada yake, Josefina, akiwa hayupo. Kwa hiyo, alijua kuwa kama asipompata, dada yake atakaporudi atamuuliza yeye. Hata hivyo, kutokana na kukosa mbinu nzuri ya mahojiano, Prospa alishindwa kupata taarifa alizozitaka kwani alimtia hasira Mustafa akashindwa kutoa ushirikiano. Baada ya kuona hivyo, nafsi yake ilimwongoza atumie mbinu ya kubembeleza, lakini nayo haikufua dafu.

Pia, utendaji kwa mtindo wa kuhoji umetumika kati ya askari na Prospa ili kupata maelezo ya namna Merisho alivyotoweka nyumbani. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

“Kijana, hebu njoo,” askari alimwita Prospa. Prospa aliulizwa jina, umri, shule anayosoma, na alikuwa wapi mtoto alipopotea. Prospa alijibu, “Wenzangu walikuja kunichukua tukacheze boli uwanjani. Nilimwacha Merisho akicheza na watoto wa jirani.” “Uligundua wakati gani kwamba mtoto amepotea?” Prospa alianza upya kueleza maelezo ya Mustafa pamoja na maneno ya mama aliyefuatana naye ... (uk. 10 - 11).

Nukuu hii inaonesha utendaji wa mahojiano uliofanywa na polisi kwa Prospa ambaye ni mhusika mkuu. Kitendo cha Prospa kuitwa na askari kinaonesha kuwa alikuwa mbali; hivyo, ilibidi asogee kwa ajili ya mahojiano hayo. Katika mahojiano haya, askari alirudia kumuuliza maswali Prospa ili apate mahali pa kuanzia uchunguzi wake. Ni kawaida kwa askari yeyote kuhoji mtu aliyeleta mashitaka katika kituo cha polisi kwa sababu hiyo. Imebainika kuwa Prospa alijibu kwa ufasaha kila alichoulizwa kwa sababu alikuwa na shauku ya kumwona Merisho. Hata hivyo, pamoja na mahojiano yote hayo, Prospa hakuona dalili ya Merisho kupatikana. Prospa alipoteza imani kwa askari kwa kuwa walikuwa wanauliza tu maswali bila vitendo. Mtindo wa mahojiano kama huu unadhihirika katika riwaya ya

Haini (2003) ambapo askari walimhoji Hamza kutokana na kifo cha Kigogo. Askari waliamini kuwa huenda akawa anajua kuhusu njama zilizopangwa, kwasababu alikuwa rafiki wa Hamduni, ambaye alikuwa ni mtuhumiwa namba moja.

Sehemu nyingine inayoonesha mahojiano ni baada ya Prospa kuanza safari ya kuelekea Dar es Salaam. Alitembea kwa miguu kwa muda mrefu, hatimaye alikutana na watoto waliokuwa wanaochunga ng'ombe. Baada ya kuwasalimia, aliwaomba maji ya kunywa, kisha aliwafuata hadi kwao. Wazazi wa watoto hao walianza kumhoji baada ya kusikia kutoka kwa watoto wao kuwa anakwenda Dar es Salaam kwa miguu kumtafuta mpwa wake aliyeibwa. Mwandishi anafafanua:

Wazazi wa wale watoto walimuuliza Prospa, “Dada yako alifanya nini kuhusu jambo hili?” Prospa alijibu, “Hofu na huzuni ilimzidia dada. Yeye aliwapelekea wazee habari, halafu akangoja matokeo ya uchunguzi wa polisi. Polisi waliuliza maswali mengi sana, lakini mtoto hakupatikana.” Waliuliza tena kama alipeleka habari kwenye redio na kwenye magazeti. Prospa alisema, “Hapana. Kwani redio na magazeti yangemtafutaje Merisho?” Yule msichana mdogo aliyekuwa akichunga ng'ombe alicheka, “Ee wewe hujui? Ukitangaza kwenye redio kila mtu Tanzania atasikia. Halafu kwenye gazeti unapeleka picha. Labda mtu angemwona amrudishe nyumbani.” Prospa hakuamini ... (uk. 42 - 43).

Katika mazungumzo haya, wazazi walihoji kwa sababu walishangazwa na safari ya Prospa. Imani ya wazazi hawa ni kutoa taarifa polisi, ambao ndio wenye dhamana ya kutafuta watu waliopotea. Pia, wazazi hawa waliona Prospa ni mdogo kufanya jukumu kama hilo, labda angelifanya mama wa mtoto, Josefina. Katika mazingira ya kawaida, ni wazi kuwa mzazi yeyote angeulizia baada ya kupata taarifa ya safari hiyo. Hata hivyo, wazazi hao

walimshauri Prospa abaki nyumbani ili wamsaidie namna nzuri ya kufika Dar es Salaam, sio ile ya kutembea kwa miguu. Hata hivyo, Prospa anaonesha kutoridhishwa na ushauri wa wazazi hao; hivyo, anaamua kutoroka ili aendelee na safari yake ya kumtafuta Merisho. Kutokana na Nadharia ya Saikochanganuzi, Prospa hakufanya busara kutoroka kwa sababu wazazi waliahidi kumsaidia kufika Dar es Salaam, lakini nafsi ya kiwango cha kati ilimsukuma kutoroka kwa kuona ni busara kwake kuendelea na safari aliyoianza. Suala la majadiliano limeshadidiwa pia na Ilomo (2017) anapoonesha mahojiano kati ya mama Resi na Tumaini katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Mama Resi alikuwa akimhoji Tumaini kuhusu mwanamke anayetaka kumuoa ambaye alikuwa hajasoma. Hata hivyo, Tumaini alikuwa haamini katika elimu bali upendo wa dhati.

Utendaji mwingine wa mtindo wa mahojiano ulikuwa baina ya Petro (kaka yake Prospa) na Prospa baada ya kukutana Manzese jijini Dar es Salaam. Prospa alishangaa sana kumwona kaka yake ambaye alikuwa hajachana nywele, suruali yake ilikuwa chafu, shati lake la rangi ya buluu halikuwa limefungwa kifungo hata kimoja, na raba alizovaa miguuni zilikuwa zimechakaa. Petro naye, alikuwa anamshangaa Prospa amefikaje jijini Dar es Salaam. Hata hivyo, Prospa, tangu anatoka Moshi, alikuwa anafahamu kuwa kaka yake anaishi Dar es Salaam sehemu iliyoitwa Manzese. Baada ya kukutana, mazungumzo yao yalikuwa kama ifuatavyo:

“Kaka Petro!” Prospa alimaka, “Sijakutambua!” “Mezea basi,” Petro alisema. “Unafanya nini Dar?” “Tumefika sasa hivi. Kwa basi. Lo! Jamani, siamini bahati hii! Nilikuwa nataka kuulizia unakoishi. Nimekuja kumtafuta Merisho.” Prospa alisema kila kitu kwa haraka, akiwa amefurahi sana. “He, unakuja kuulizia mtu jijini hapa? Unafikiria huku ni Kiboriloni?” Petro alisema, huku akiangalia huku na kule.

Prosipa alimtaazama kaka Petro kwa mshangao, kama bado hajaamini kwamba macho yake yanamwambia kweli. “Habari za Moshi?” Petro aliuliza. Akili ya Prosipa ilikuwa imetekwa nyara na habari za kupotea kwa Merisho, kwa hiyo alijibu, “Aliibwa, nimekuja huku kumtafuta.” “Kumtafuta nani? Mimi? Petro aliuliza akiwa anacheka (uk. 58 - 59).

Katika dondoo hili, utendaji wa kuhoji unatudhihirishia kuwa Prosipa alipata furaha kubwa mara baada ya kukutana na kaka yake. Kutokana na furaha hiyo, alijikuta anajibu swali ambalo hajaulizwa. Aliamini suala la Merisho kupatikana limekuwa jepesi kwa kuwa Petro ni mwenyeji katika jiji hilo. Kwa upande mwingine, Petro alishangazwa na ujio huo, jambo ambalo lilimfanya amhoji. Lema (2020)² anasema kuwa Prosipa alikuwa na bahati sana kukutana na kaka yake, aliona ni mwanga katika kumtafuta Merisho. Mawazo ya Lema yanathibitisha taharuki ya Petro, aliyeshangazwa na maneno ya Prosipa kuhusu kumtafuta katika jiji kubwa na lenye watu wengi kama Dar es Salaam.

Utendaji kwa mtindo wa kushawishi

Wahusika hutumia mazungumzo kama nguzo kuu ya kuonesha utendaji wao. Aidha, mbali na kuhoji, utendaji uliooneshwa na wahusika kwa njia ya mazungumzo ulifanywa pia kwa minajili ya kushawishi. Ushawishi hufanywa ili kupata kitu fulani kama chakula, mavazi, na usafiri. Mazungumzo ya namna hii huhitaji mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulia machozi, kuonesha sura ya huruma, kuongea kwa sauti ya chini, pamoja na kudanganya. Mathalani, baada ya Prosipa kupanga mipango yake ya kwenda Dar es Salaam kumtafuta Merisho, aliwaza namna ya kutoka

² Mahojiano kati ya mtafiti na Bi. Elieshi Lema yalifanyika katika ofisi ya mtaalamu huyu iliyopo katika jengo la kampuni ya uchapishaji ya E&D, Sinza Africasana, jijini Dar es Salaam mnamo tarehe 17/02/2020. Lema ni mmiliki mwenza wa kampuni hiyo na mwandishi wa vitabu mbalimbali vya watoto

katika geti la TPC kwa sababu alikuwa akifahamika. Hata hivyo, alipokaribia getini, aliona gari aina ya *pick-up* likipakia majani. Prospa aliona ni bahati kwake na kuamua kuomba lifti baada ya kumsalimia dereva ambaye hakuitika. Dereva alimkatalia kwa kumwambia kuwa gari lilikuwa limejaa. Prospa hakuridhika na majibu ya dereva, ikambidi amshawishi kwa kudanganya. Mwandishi anasema:

“Bibi anaumwa kaka nampelekea...” Prospa alianza kukariri haraka

“We mtoto huoni gari imejaa? Hakuna nafasi,” dereva alisema kwa sauti isiyokuwa na subira.

“Bibi anaumwa, nampelekea dawa,” Prospa aling’ang’ania akawa ameshika gari kama vile ataweza kulikataza kuondoka. Nikiondoka hapa! Nikiondoka hapa tu, nitakuwa nimeokoka, Prospa alijiambia kimoyomoyo.

Dereva alipiga gari moto.

Prospa aling’ang’ania gari “Kaka...,” alisihi.

“Shauri yako, panda,” dereva alisema huku akiondoa gari.

Prospa alitupa mkoba kwenye majani ndani ya gari halafu akarukia ndani huku gari tayari limekwishaanza kuondoka (uk. 21 - 22).

Katika dondoo hilo, tunaoneshwa kuwa kutokana na ushawishi wa Prospa ulioambatana na uongo, aliweza kupata lifti ambayo ilimtoa katika maeneo aliyokuwa akifahamika; hivyo, alijihisi yupo salama. Kulingana na Nadharia ya Saikochanganuzi, Prospa alisukumwa na nafsi ya kiwango cha ukomavu ambayo inachunguza uadilifu wa tendo la wema na ubaya wake kabla ya kulitenda. Aliona uongo sio mzuri, lakini, kwa wakati, ule hakuwa na njia nyingine zaidi ya kudanganya ili atoke eneo hilo na kwenda kumtafuta Merisho.

Halikadhalika, Sara alitumia ushawishi ili Prospa aende kunywa supu pale walipokutana. Prospa alikuwa na hofu kwa sababu ilikuwa mara ya kwanza kuonana na binti huyu. Katika mazingira ya kawaida, huwa ni vigumu mtu kukubali apewe chakula chochote na mtu asiyemfahamu vizuri. Mathalani, katika vyombo vya usafiri wa umma, wasafiri hutangaziwa kutokukubali kupokea chakula kwa mtu asiyefahamika hata kama wamekaa katika kiti kimoja. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa Sara alihisi kuwa Prospa ana njaa kwa sababu ilikuwa ni asubuhi. Mwandishi anatanabaisha hili kwa kusema:

Msichana alisema, “Twende tukanywe thupu.” Prospa alitingisha kichwa kukubali lakini hakuondoka kumfuata. Alimtaazama hadi alipoingia ndani ya *Same Guest House and Bar*. Msichana alirudi mara moja, akanawa uso wake palepale aliponawa Prospa, halafu akamfuata na kumshika mkono. Prospa aliogopa. Msichana alimwambia, “Twende kwetu.” “Siwezi. Nakwenda Darisalam,” Prospa alijibu. “Kweli? Na mimi nataka kwenda Darithalam.” Msichana alisema. “Twende wote. Thiku thote natamani kwenda kutembea Darithalam. Nataka nithome univethiti.”... (uk.48).

Nukuu hii inatuthibitishia kuwa Sara alitumia utendaji wa ushawishi ili Prospa akubali kuambatana naye. Utafiti umebaini kuwa, ijapokuwa watoto hawa walikutana kwa mara ya kwanza, ushawishi wa Sara ulifanikiwa. Sara aliongozwa na nafsi ya kiwango cha kati (*Ego*) kumshawishi Prospa anywe supu kabla ya kuondoka.

Ushawishi pia ulitumika pale ambapo Sara alikuwa anaomba lifti kuelekea Dar es Salaam. Baada ya Sara na Prospa kukutana, Prospa alimweleza lengo lake la kwenda Dar es Salaam. Sara alijitolea kumsindikiza akimwambia kuwa alitamani kwa muda mrefu kwenda Dar es Salam ili akasome Chuo Kikuu. Ijapokuwa Sara alipenda kuitwa Edison, Prospa alimpa masharti

kuwa akiomba lifti atamuita jina hilo. Sara alijaribu kusimamisha magari, lakini yaliwapita. Baada ya kujaribu kwa muda mrefu, gari moja lilisimama. Mwandishi anasema:

Sara alimshika Prospa kwa nguvu na kumwambia, “Acha niombe mimi. Uthitheme kitu.” “Usipoipata utanikoma,” Prospa alimtishia. Sara alimwambia mwenye gari, “Baba, tunatembea mimi na mdogo wangu kwenda Darithalam. Tuthaidie.” “Mnatembea? Mmetoroka nyumbani?” Mwenye gari aliuliza. Mkono mmoja wa Sara ulimfinya Prospa asije akasema kitu. Sara alisema, “Baba yetu yupo Darithalam, thatha mama ametukimbia, amemfuata baba. Nyumbani hakuna chakula.” “Lo! Nyie watoto mnasema kweli?” Mwenye gari aliuliza. Prospa alidakia, “Hapana baba, ni kweli kabisa.” “Ingieni,” mwenye gari alisema akawafungulia mlango ... (uk. 51 - 52)

Hapa, mwandishi ameonesha namna Sara alivyomshawishi dereva kwa kumdanganya kuwa Prospa ni mdogo wake na walikuwa wanaelekea Dar es Salaam kwa wazazi wao. Kutokana na uongo huo, dereva alishawishika na kuwabeba katika gari lake. Kwa hiyo, lengo la Sara kuomba lifti lilikuwa waondoke, pia ili aitwe Edison. Kutokana na nafsi ya tatu ya Nadharia ya Saikochanganuzi, Sara alichunguza uadilifu wa tendo la kudanganya kabla hajalitenda. Kwa kuwa uongo ni kinyume na maadili, lakini kama uongo unaokoa, wakati mwingine, inabidi utumike.

Ushawishi pia umetumiwa na Prospa kwa kaka yake, Petro, alipokuwa anataka ampeleke kwake au kwa mjomba wao, Feliksi. Ijapokuwa walikutana katika mazingira ya kutatanisha na kila mtu akiwa na shughuli zake, Prospa hakulijali hilo. Ilibidi atumie mbinu ya kumshika mkono kaka yake ili kumzuia apate kile alichotaka. Hili linafafanuliwa na mwandishi kama ifuatavyo:

“Sasa unaishi wapi kaka? Nakuomba unipeleke nyumbani basi,” Prospa alimsihi kaka yake. Alimshika mkono kama kumzuia asiondoke. “Yaani umekuja kwangu?” Petro aliuliza. “Nilikuwa nataka ... Utanipeleka kwa mjomba Feliksi basi,” Prospa alisihi. “Mambo ya kushtukiza siyawezi mie,” Petro alilalamika. “Kaka Petro jamani,” Prospa alisema kwa sauti ya unyonge. “Agh! Balaa gani hii,” Petro alilalamika, akionesha kukasirika. “Basi twende,” alisema kwa ghadhabu. Waliondoka pamoja na kuelekea kwenye uchochoro mmoja katikati ya nyumba nyingi zilizosongamana (uk. 60).

Katika nukuu hii, tunaonesha utendaji wa ushawishi kupitia Petro na Prospa. Ni jambo la kawaida mtu anapokuwa na jambo lake la lazima kutumia kila njia kuhakikisha analifanikisha. Prospa alifika Dar es Salaam, lakini alikuwa hajui ni wapi atalala na atanzaje kumtafuta Merisho. Hata hivyo, Petro alighadhibika, lakini alikubali kuwapeleka sehemu anayoishi baada ya kushawishiwa. Lema (2020) anasema kuwa, pamoja na maisha magumu yanayothibitishwa na mwonekano wa Petro, alikuwa na sehemu ya kulaza ubavu wake giza linapoingia. Hili linathibitishwa katika riwaya hii kuwa Petro alikubali kuwapeleka sehemu anayoishi, kwenye nyumba iliyokuwa kwenye bonde, mwisho wa uchochoro. Kwa hiyo, lengo la ushawishi wa Prospa lilitimia.

Sehemu nyingine inayoonesha utendaji wa wahusika kwa mtindo wa ushawishi ni baada ya Sara na Uzuri kukutana. Kwa kuwa lengo la kumkutanisha Sara na Uzuri ni kupata taarifa zitakazosaidia kumpata Merisho, rafiki zake Sara walimwacha ili ajenge urafiki naye. Uzuri hakumpenda Sara, lakini Sara alimshawishi kwa maneno mazuri ya kumsifia. Mwandishi anasema:

Sara na Uzuri walikaa kimya. Sara alikuwa akifikiria jinsi ya kumwingia Uzuri bila kumkasirisha. Uzuri alikuwa anachambua mchicha ... Hakutaka msichana huyu akae naye jikoni, kwani angechelewesha kazi yake tu. Mwishowe alimuuliza Sara, “Sasa wewe unasubiri nini hapa? Nenda ukakae na hao wazururaji wenzako.” Sara alitabasamu, mlango wa mazungumzo umefunguka, alijiambia kimoyomoyo. Sara akicheka uso wake hung’aa na kuonesha uzuri wake kamili. Meno yake yalikuwa meupe mithili ya mahindi mapya. Uzuri alimtazama, alivutiwa na tabasamu, na hapo hapo kabla Uzuri hajasema lolote, Sara alisema, “Wewe ni mthuri kama udi.” Uzuri aliuliza, “Unasemaje?” “We ni mthuri kama udi.” Sara alirudia. Uzuri alicheka. Alirudia tena kuchambua mchicha. Lakini kicheko kilimbana akaanza kucheka tena. “Mtoto we una mambo,” alisema ... Sasa wote wawili walicheka. Uzuri alimwambia Sara, “Nisaidie basi kuchambua mchicha.” (uk. 141 - 143).

Katika nukuu hii, ushawishi wa Sara uliweza kumchota Uzuri wakawa kitu kimoja. Sara alimsaidia Uzuri kazi za jikoni na baadaye kumsuka nywele zake. Hivyo, Uzuri alimwamini Sara na kuzungumza mambo mengi ambayo mengine Sara alikuwa anayataka. Kwa mfano, alielezea kuhusu Awaichi ambaye aliiba mtoto wa kaka yake huko Moshi kwa sababu ana watoto wa kike tu. Bila kuwa na urazini kwamba Sara alifika katika jiji hilo kwa ajili ya kumtafuta mtoto huyo, Uzuri alieleza kila kitu hata mahali alipofichwa.

Utendaji kwa mtindo wa kujifunza

Aina hii ya utendaji hudhihirika pale ambapo mhusika mkuu hujifunza mambo mbalimbali kutokana na kuwa karibu na watu na kuzungumza nao. Mathalani, baada ya Prospa kuingia Dar es Salaam na kukutana na changudoo, alijiunga nao katika maisha ya mitaani. Walizunguka katika mitaa mbalimbali na kulala nje ya maduka makubwa kila ilipofika usiku.

Kitanda chao kilikuwa maboksi yaliyokuwa yamefungiwa vitu mbalimbali. Kutokana na mazungumzo ya vijana hawa, Prospa alijifunza kazi mbalimbali kama kubeba mizigo, kuosha magari, kufanya usafi katika hoteli mbalimbali na kujaza maji mapipa ili wapate riziki kama vile chai ya asubuhi. Mwandishi anasema:

Walipofika mnara wa saa walipinda kulia wakafuata mtaa wa India. Walitembea moja kwa moja hadi barabara ya Umoja wa Wanawake, wakavuka, wakaingia bustani ya Mnazi Mmoja wakaendelea hadi Kariakoo. “Hizi ndizo sehemu za kupatia chakula. Chai asubuhi na chakula cha jioni. Huku watakupa kazi kufagia hoteli au kuosha vyombo halafu unapata chakula,” Mansa alieleza. “Huku ukiomba hupati kitu,” Tofa aliongeza. “Ukiomba nini?” Prospa aliuliza. “Pesa.” Kama hivi: Saidia mama, naomba hela ya chakula mama. Nasikia njaa mama, sijala kitu tangu jana... Hivyo.” Tofa aliigiza ili Prospa aelewe vizuri (uk. 118).

Dondoo hilo linatuonesha kuwa, kutokana na kukutana na watoto wa mitaani na mizunguko waliyoifanya katika jiji la Dar es Salaam, Prospa alijifunza mambo mengi. Lema (2020) anasema kuwa watoto wa mitaani wana uwezo sawa na watoto wengine isipokuwa wamekosa mtu wa kuwalea, kuwaelekeza na sehemu maalumu ya kulala. Anaongeza kuwa matukio yote ya watoto wa mitaani aliyashuhudia mwenyewe katika mitaa mbalimbali ya Dar es Salaam wakati anakiandaa kitabu hiki.

Vilevile, Sara na Prospa walipofika Zanzibar, walikwenda nyumbani kwa Mzee Mohamed na Bibi Fatuma. Wenyeji wao waliwakaribisha na kukaa nao kwa siku tano. Walieleza lengo lao lililowaleta. Bibi Fatuma alistaajabu kusikia mtoto wake alijaaliwa kupata mtoto. Kwa muda waliokaa na wazee hawa, Prospa na Sara walifundishwa mambo mbalimbali. Mwandishi anasema:

Sara alijifunza kuweka ukili rangi ...Walitembea shambani na Bibi Fatuma, akamwonesha mti wa mdaa, akamfundisha jinsi ya kutoa vipande vya gamba lake. Alimwonesha pia mmea unaoitwa manjano, jamii ya tangawizi na binzari, akamwonesha jinsi ya kupaka mizizi yake ... Halafu alijifunza kusuka mkeka wa kuchanganya rangi tofauti ... Prospa alijifunza kukwea miti mirefu. Alifahamu jinsi ya kuangua mafenesi manene, jinsi ya kuyala, mafenesi yenye utamu wa sukari (uk.101).

Nukuu hii inadhihirisha kwamba muda waliokaa Zanzibar ulikuwa darasa tosha kwa Sara na Prospa. Ujuzi walioupata ni msaada kwa maisha yao ya baadaye. Hata hivyo, utafiti ulibaini kuwa wepesi wa akili zao kushika vitu ulikuwa ni msaada wa kujifunza yote. Jambo hili linashadadiwa na Lyimo (2020)³ anaposema kuwa wepesi wa Sara na Prospa katika kukabiliana na mazingira mapya kuliwafanya wajifunze mambo mengi kwa muda mfupi.

Utendaji kwa mtindo wa kujenga maelewano

Maelewano ni jambo la msingi katika kujenga uhusiano. Mara nyingi, ni vigumu kuwa na uhusiano na mtu bila kufahamiana naye; hivyo, watu wengi hujitahidi kumfahamu mtu ili kuongeza uhusiano huo. Uchunguzi wetu umebaini kuwa wahusika nao hutumia mazungumzo ya kiutendaji kama nyenzo ya kujenga maelewano ili kufanya mambo mbalimbali kwa pamoja. Mwandishi wa riwaya iliyoachambuliwa ameyaonesha hayo katika sehemu mbalimbali za riwaya yake. Mathalani, wakati Prospa alipofika Same, hakutarajia kukutana na msichana huyu na wala hakutaka aende naye kumtafuta Merisho. Lakini, kutokana na mazungumzo yao yaliyoambatana

³ Mahojiano kati ya mtafiti na Dkt Lyimo yalifanyika katika ofisi ya mtaalamu huyu iliyopo katika jengo la TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mnamo tarehe 17/06/2020. Lyimo ni Mhadhiri, ambaye alikuwa mkuu wa idara ya IFAM na mtaalamu wa fasihi ya watoto.

na ucheshi wa Sara, waliweza kufahamiana na kuambatana pamoja kwenda kumtafuta Merisho kama inavyoelezwa na mwandishi:

Kabla hajafika pale, alikutana na msichana aliyeelekea hukohuko Same *Guest and Bar*. Msichana alijifunga kitenge kifuni juu ya matiti. Alikuwa amebeba kichwa cha ng'ombe aliyechinjwa, bado damu inadondoka. "Yesu." Prospa alishtuka akataka kukimbia. Alishika mdomo kwa mshangao. Msichana alisimama na kumwalia Prospa, halafu alicheka sana. "Mungu wangu," Prospa alizidi kushangaa, akionesha uso wa kustaajabu na hata kuogopa. Msichana akiwa na sura ya ucheshi, aliuliza, "Ee nini? Prospa hakujibu. Aliendelea kustaajabu msichana ambaye jicho lake la kushoto lilikuwa bovu ... Msichana alisema "Twende tukanywe thupu." Prospa alitingisha kichwa kukubali lakini hakuondoka kumfuata ... (uk. 47 - 48).

Kwa hiyo, kutokana na mazungumzo haya, utafiti umebaini kuwa Prospa na Sara walijenga maelewano yaliyowafanya kuwa kitu kimoja: wakafahamiana, wakanywa supu pamoja na baadaye wakaondoka kuelekea Dar es Salaam. Masimulizi yanaonesha hata walipofika Dar es Salaam, waliendelea kuwa pamoja na kuelewana katika kumtafuta Merisho hadi kumpata. Suala la kujenga maelewano linatiliwa mkazo na Ricard (2000) anaposema kuwa mazungumzo huwafanya watu waelewane na kufikia muafaka wa kile wanachokihitaji. Anatolea mfano suala la migogoro katika jamii, kwamba suluhisho pekee la kutatua migogoro ni kukaa pamoja na kuzungumza. Mazungumzo hayo yanaweza kuleta muafaka kama pande zote mbili zitaelewana.

Sehemu nyingine inayofafanua mazungumzo kwa mtindo wa kujenga maelewano pale Prospa na Sara walipotoka Zanzibar na kujipumzisha katika bustani. Kwa sababu ya uchovu waliokuwa nao, walipitiwa na usingizi. Waliposhtuka, waligundua kuwa wameibiwa kila kitu

walichokuwanacho. Wakati wanaendelea kushangaa na kuulizana hili na lile, waliona kundi la watoto likija upande wao wakiwa wameshika chupa mikononi. Prospa na Sara walishtuka, walijikuta wameshikana bila kupanga. Kutokana na ugeni wao katika eneo hilo, Prospa na Sara waliogopa sana. Kundi la watoto watatu liliwakaribia na mmoja wao akawaambia kuwa hawaruhusiwi kulala ovyoovyo kama vitoto kwa sababu wanaweza kuuawa. Kauli hii ilifungua mazungumzo kati yao kama mwandishi asemavyo:

Prospa alisema, “Huyu ni Sara. Huyu Sara ni dada yangu, ni mdogo wangu. Sara ni bubu, hawezi kuongea.” “Mlifika lini mjini hapa,” mvulana mwingine aliuliza. “Jana, leo.” Prospa alijibu. Tunamtafuta Merisho. Merisho ni mpwa wangu alipotea kule TPC. Unafahamu mahali panapoitwa TPC? Kile kiwanda cha sukari? Sasa Merisho hayupo Moshi, wala Manzese, wala hayupo Zanzibar, tumeshatoka huko.” Prospa aliongea kwa haraka... alitaka wamwonee huruma wasiwaumize. “Thithi tumeibiwa vitu vyetu vyote. Hatuna petha. Thithi ni mathkini,” Sara alisema. Wavulana wote watatu waliangua kicheko. Walicheka sana. Msemaji wao alisema kwa sauti ya kike iliyomuigiza Sara huku akicheka. “Tumeibiwa malithetu thote. Thithi tulikuwa matajiri wakubwa, tulikuwa tukiishi mathaki!” wavulana waliangua kicheko. Walikuwa wanafurahia wasiwasi na hofu yao. Prospa na Sara walicheka pia ingawa kwa wasiwasi (uk. 111 - 113).

Kutokana na mazungumzo katika nukuu hiyo, utafiti umebaini kuwa, ijapokuwa vijana hawa walikuja kwa ukali uliojenga hofu na wasiwasi kwa Sara na Prospa, maongezi yao ya ucheshi na utani yalifungua ukurasa mpya wa maelewano. Pia, kutokana na maongezi hayo, Sara alijikuta anaongea ili watoto wale wawaonee huruma, na kusahau kuwa alitambulishwa kuwa yeye ni bubu. Kutokana na nafsi ya pili ya Nadharia ya Saikochanganuzi, Sara aliona ni jambo la busara kuongea ili waonewe huruma. Hata hivyo,

woga wa Sara na Prospa uliisha na kujiona ni sehemu ya vijana hao, walielewana kwa kiasi kikubwa. Baadaye, walikuwa kitu kimoja, wakasaidiana, kushauriana katika maisha yao ya mitaani, na kumtafuta Merisho hadi kumpata. Lema (khj) anasema kuwa:

Watoto wa mitaani wana upendo mkubwa sana kati yao na wanaelewana kuliko watu wanavyodhani. Katika mitaa niliyopita, nililishuhudia hili. Mathalani, kuna mtaa niliwakuta wanapika pamoja, wana viongozi wao, ambao wana sauti na amri kama walivyo wazazi nyumbani. Pia, wana vikundi vyao vyenye malengo mbalimbali na hutofautiana kutoka kundi moja na jingine.

Maelezo ya Lema yanashadadia maelewano waliyonayo watoto wa mitaani. Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa vikundi hivyo ni kama sehemu ya familia zao walizojiundia na kupeana majukumu.

Utendaji kwa mtindo wa kuamuru

Kwa mujibu wa Bakhressa (1992), kitenzi amuru kina maana ya kuamrisha; toa maagizo, amri, maelekezo. Wahusika wakuu katika riwaya hii huamuru au huamuriwa na watu wengine kufanya jambo fulani. Amri hizi hutokana na mmoja wa wahusika kusita kufanya jambo fulani au kukataa kabisa. Katika mazingira ya kawaida, amri hutoka ili kukidhi matakwa ya watawala au wakubwa, na, kwa kawaida, amri inapotolewa, huwa ni sharti itekelezwe. Baada ya Prospa kukutana na Sara pale Same, walifahamiana, na Sara akaomba kuambatana na Prospa kwenda kumtafuta Merisho. Prospa alionesha kumshangaa na kumwogopa Sara ambaye alikuwa na jicho bovu. Katika hali asiyoitarajia, Prospa alijikuta anapewa amri na Sara ili kutekeleza azma ya kwenda pamoja Dar es Salaam. Kwa mfano,

alimwamuru amsubiri ili aende akachukue nguo. Pia, alimwamuru kuweka nguo katika mkoba wake. Mwandishi anasema:

Msichana alisema, “Thikia, mimi nitakwenda nyumbani kuchukua nguo. Ningoje hapa. Uthiondoke. Ukiondoka nitakupata tu.” Alicheka kwa furaha. Jicho lake la kulia liling’aa. Aliondoka pale akikimbia kuelekea kilimani ... Msichana alirudi akikimbia. Alikuwa amevaa gauni. Mkononi alikuwa na kifurushi kidogo sana. “Nini hicho?” Prospa aliuliza kwa wasiwasi. “Kitenge. Weka kwenye mfuko,” msichana aliamuru. Prospa alisita. Alitamani kumwambia akifungue hicho kitenge, akikung’ute ili ahakikishe kwamba hakufungia vitu vya kichawi. Msichana hakuwa na subira. Alisema, “Agh, hebu,” Akachukua mkoba wa Prospa aliokuwa ameuning’iniza begani, akafungua zipu, akaweka kitenge chake bila kutazama ndani. Alifunga zipu, akaning’iniza mkoba begani mwa Prospa. Halafu akasema, “Thatha tukanywe Thupu.” (uk. 48 - 49).

Katika dondoo hilo, utendaji wa kuamuru uliofanywa na Sara ulisababisha Prospa kutii kila anachoambiwa, ijapokuwa alikuwa na wasiwasi mwingi. Aliwaza kumkimbia msichana huyu, ingawa hakufanikiwa. Imebainika kuwa Prospa alimhitaji Sara katika kipindi hicho na alimwona kama mkombozi ndiyo maana alitulia na kutii. Hata hivyo, imebainika kuwa, endapo Sara asingeweza kumwamuru Prospa, huenda asingefanikiwa azma yake ya kwenda Dar es Salaam. Bakize (2020) anabainisha suala hili kwa kusema kuwa mwandishi wa riwaya hii ameungana na waandishi wengine wanaopingana na suala na kumdunisha mwanamke. Anaongeza kuwa Sara alikuwa na amri kwa watoto wenzake na walitii bila kujali jinsia yake. Mtaalamu huyu alitolea mfano namna Sara alivyowaamuru watoto wenzake waondoke kwa sababu walikuwa wanamuuliza sana maswali. Kwa hiyo, ni

dhahiri kuwa suala la kuamuru haliangalii jinsia kwa kurejelea mawazo ya Bakize.

Sehemu nyingine inayoonesha utendaji wa kuamuru ni baada ya Prospa na Sara kukutana na changudoo katika bustani waliyokuwa wamepumzika. Walieleza azma yao ya kuwepo katika jiji la Dar es Salaam kuwa ni kumtafuta mpwa wake Prospa, ambaye alipotea nyumbani kwao, TPC - Moshi. Kiongozi wa changudoo aliwaeleza kuwa, kwa kuwa wao ni changudoo, basi Prospa na Sara kuanzia wakati huo nao ni changudoo. Hivyo basi, aliwaamuru kuacha kulialia na kulala ovyo. Kiongozi huyo pia alimwamuru Tofa (mmoja kati ya changudoo) amchukue Sara ampeleke kwa dada yao. Mwandishi anaeleza:

“Sasa wewe Tofa, mchukue Sara, bubu anayeweza kuongea, mpeleke kwa dada yao. Yeye atajua la kumfanya. We, Mansa, huyu wako. Mpe jina kama hana lake,” mkubwa wao aliamuru. Prospa alijaribu kukataa. Alijaribu kumtoa Sara mikononi mwa Tofa. Msemaji wao alimwonesha kipande cha chupa kilichochongeka na kusema, “Ninyi hamjui jiji hili. Jiji halina huruma hili, na tukiwaacha mnaweza kuumizwa vibaya. Tushaamua ninyi ni changudoo kuanzia sasa. Wasichana wana shughuli zao na sisi zetu. Ukileta fujo tutakuumiza.” Bila maneno zaidi, wala ubishi kutoka kwa yeyote, yule mvulana kiongozi alianza kuondoka na kundi zima likamfuata. Prospa na Sara walitembea katikati yao kama mateka ... (uk. 113 - 114).

Katika nukuu hii, amri ya kiongozi huyo haikupingwa na yeyote. Na aliyejaribu kupinga alipata vitisho. Kwa hiyo, walitekeleza yote waliyoambiwa. Hivyo, Prospa na Sara wakawa miongoni mwa changudoo katika jiji la Dar es Salaam, wakalala na kuamkia barabarani. Hata hivyo, umoja wao ulikuwa na tija kubwa katika madhumuni yao ya kuja Dar es

Salaam, hatimaye walifanikiwa kumpata Merisho. Kulingana na Nadharia ya Saikochanganuzi watoto hawa waliongozwa na nafsi ya kiwango cha ukomavu kutii kila walichoambiwa ili kufanikisha lengo lao lililowapeleka katika jiji la Dar es Salaam.

Utendaji mwingine wa mtindo wa kuamuru ulitolewa tena na kiongozi wa changudoo baada ya kujadiliana na wenzake namna ya kumpata Merisho. Watoto hawa walikuwa wamehifadhiwa nyumbani kwa mjomba wake Prospa, Feliksi. Lengo lao kubwa lilikuwa kujua mahali anapoishi mzee Matayo, na walihofia wakipelekwa na Uzuri, mambo yataharibika. Katika majadiliano yao ilionekana haja ya Sara kupelekwa hapo ili asaidie kuongea na Uzuri mpaka amwoneshe kwa Mzee Matayo. Kutokana na umuhimu huo, kiongozi wao aliamuru:

“Lazima tumpate Merisho, kwa bidii yetu wenyewe. Sasa majadiliano yaishe. Tofa we nenda ukamlete Sara. Ondoka na Prospa. Mweleze dada yao kwamba tunamhitaji Sara leo hii. Mwambie kwamba ni lazima aje Sara na siyo msichana mwingine. Mimi nitabaki hapa niongee na mzee Mateo.”... “Tofa, nenda kwa Uzuri, na Prospa nenda kwa Mateo. Tumieni maarifa mpate nauli. Mimi nitaangalia humu ndani kama kuna chochote.” Maelezo ya Mansa yalikuwa ni sharia waliyoifuata bila ubishi mwingi (uk. 138 - 139).

Katika nukuu hii, kiongozi aligawa majukumu, lakini kwa kutumia amri. Kutokana na amri hii, walifanikiwa kupata kiasi cha shilingi elfu moja na mia tatu; hivyo, Prospa na Tofa walipewa na kiongozi wao shilingi mia tatu kwa ajili ya nauli, na pesa iliyobaki waliweka ili iwasaidie baadaye. Hivyo, Tofa na Prospa waliondoka kuelekea mjini kumfuata Sara, wakamleta nyumbani kwa Feliksi. Lengo lao lilikuwa kumtumia Sara ili amshawishi Uzuri apate habari zitakazosaidia Merisho kupatikana.

Hitimisho

Makala hii imejadili mitindo mbalimbali ya utendaji wa wahusika wa fasihi ya watoto ya Kiswahili. Imebainika kuwa utendaji wa wahusika hao unadhihirika kupitia lugha ya mazungumzo kwa kiasi kikubwa na masimulizi ya mwandishi kwa uchache. Mitindo hiyo ya utendaji imewawezesha wahusika kufanikisha safari yao ya kumtafuta Merisho hadi kumpata. Riwaya ya *Safari ya Prospa* imetumika kurejelea utendaji huo kwa kutumia wahusika wake wakuu, Prospa na Sara, ambao walifanya mazungumzo wao kwa wao, au wao na wahusika wengine. Matokeo yanaonesha kuwa utendaji umeweza kutumika kwa mtindo wa kuhoji, kushawishi, kujifunza, kujenga maelewano, na kuamuru. Makala hii imeongeza maarifa katika fasihi ya Kiswahili kwa kutambulisha utendaji wa wahusika wakuu katika riwaya, hususani riwaya za watoto.

Marejeleo

- Bakhressa, S.K. (1992). *Kamusi ya Maana na Matumizi*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Bakize, L.H. (2013). Changamoto Zinazoikabili Fasihi ya Watoto Nchini Tanzania. *Kiswahili*, 76, 61- 71.
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Dar es Salaam and Nairobi: Oxford University Press.
- Huitt, W. & Hummel, J. (2003). Piaget Theory of Cogninitive Development. *Interactive Educational Psychology*, 3(2).
- Iloimo, L.F. (2017). Mbinu za Ujenzi wa Wahusika na Usawiri wa Sifa Zao: Uhakiki wa Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo ya E. Kezilahabi. *Mulika*, 34, 38 - 50.
- Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques* (Second Rev). New Delhi: New Age International (P) Limited.

- Lema, E (2004). *Safari ya Prospa*. Dar es Salaam: E&D Limited.
- Mbarouk, S.S. (2019). Uchambuzi wa riwaya ya *Kiu* kwa kutumia nadharia ya Saikolojia Changanuzi. *Eastern African Literary and Cultural Studies*. DOI:10.1080/23277408.2018.1540127. Iliyosomwa tarehe 21/01/2020.
- Mbunda, F.L. (1996). *Mbinu za Kufundishia Lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mlaga, W.K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.
- Mlama, P. (1981). Digubi: A Tanzanian Indigeneous Form. *The Drama Review*, 25, 4.
- Munyioki, A.M. (2018). Utendaji wa Kidrama wa Riwaya ya *Haini* ya Adam Shafi 2003, (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Moi.
- Njogu, K. & Chimerah, R. (1998). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. & Wafula R.M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jommo Kenyatta Foundation.
- Nkwera, F.M.V. (1989). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Nyambura, K. (2014). Utendaji katika Tamthiliya Sudana na Kimya Kimya Kimya (Tasinifu ya Uzamili, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Shafi, A. (2003). *Haini*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Ricard, A. (2000). *Ebrahim Hussein: Swahili Theatre and Individualism*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Vice, S. (1990). *Ed. Psychoanalytic criticism: A reader*. London: Polity Press.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi, Kenya: Vide Muwa Publishers Limited.

Wa Thiong'o, N. (1986). *Decolonising the Mind: The Language of African Theatre*. Nairobi: Heinemann Kenya.